



## TAARIFA KWA UMMA

OWM-TAMISEMI inawatangazia majina ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi kwa mwaka 2015. Wanafunzi waliochaguliwa ni kutoka shule za Serikali na zisizo za Serikali. Jumla ya wanafunzi **55,003** wakiwemo wasichana **23,303** na wavulana **31,700** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa **29,744** wakiwemo wasichana **11,450** na wavulana **18,294** sawa na asilimia **54.08** watajiunga na masomo ya Sayansi na Hisabati; na wanafunzi **25,259** wakiwemo wasichana **11,853** na wavulana **13,406** sawa na asilimia **45.92** wamechaguliwa kusoma masomo ya Sanaa na Biashara.

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2015 wataanza muhula wa kwanza tarehe **18 Julai, 2015** na hakutakuwa na fursa ya mabadiliko yoyote ya shule. Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti katika shule walizopangwa kwa wakati. Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti kwa zaidi ya siku **14** kuanzia tarehe ya mwisho ya kuripoti, nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi mwaka 2015 inapatikana kwenye tovuti ya OWM-TAMISEMI ya [www.pmoralg.go.tz](http://www.pmoralg.go.tz)

Imetolewa na Katibu Mkuu,

# OWM-TAMISEMI